TANGAZO LA SERIKALI NA. 451 la tarehe 7/7/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MAKUTUPORA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Makutupora ya mwaka 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango kwenye eneo katika Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

## JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba T23700 yenye majira – nukta 737354MS, 9376642KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo

*Tangazo La Serikali Na. 451 (linaendelea)*

wa KS 85° 18' MG kwa umbali wa kilomita 17.47 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba T23701 yenye majira – nukta 735888MS, 9359238KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG 94° 17'MG kwa umbali wa kilomita 4.28 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba T23702 yenye majira – nukta 731803MS, 9358328KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ 15° 91' MS kwa umbali wa kilomita 4.53 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba T23703 yenye majira – nukta 730406MS, 9362667KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG57° 57'MG kwa umbali wa kilomita 4.0 hadi kwenye alama ya mipaka ya upimaji namba T23704 yenye majira – nukta 724907MS, 9366279KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ87° 92' MS kwa umbali wa kilomita 6.55 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba T23705 yenye majira – nukta 725280MS, 9376652KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ00° 00' kwa umbali wa kilomita 10.36 hadi ulipoanzia.

Dodoma, ANGELINE S.L. MABULA
28 Juni, 2023 *Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.*